

Ushairi na Umoja wa Kitaifa

Vifu Makoti

Chuo Kikuu cha Machakos, Kenya

Ikisiri

Ushairi ni utanzu mkongwe wa fasihi. Ulianza na binadamu mwenyewe alipobuni lugha (Fischer, 1953). Inadaiwa kuwa binadamu alianzisha ushairi alipovumbua lugha. Baada ya maendeleo ya mwanadamu, utanzu huu ulijijengea lugha ya kipekee ambayo ni ya mvuto na kunata. Kupitia lugha hii faida nyingi zinaweza kupatikana kwa matumizi yake. Faida mojawapo ni kuhamasisha jamii ya Wakenya kukubaliana, kuvumiliana na kupendana. Mtazamo huu unaleta umoja wa kitaifa ambao unahitajika sana nchini Kenya. Kenya imekuwa na tabia ya mgawanyiko mkubwa kila wakati wa uchaguzi mkuu na baada ya uchaguzi huo. Jambo hili lilitokea 2007/8, 2013 na 2017. Kuna njia nyingi za kukubaliana na tatizo hili. Mojawapo ni matumizi ya ushairi ulio na lugha ya nguvu sana inayowagusa watu katika sherehe na hafla mbalimbali. Unaweza kutumika kama nyimbo, maghani au katika maandishi. Utafiti huu kwa hivyo, unalenga kuchunguza ushairi unavyoweza kuchangia kuunganisha Wakenya wa jamii mbalimbali wanaoongea lugha tofauti tofauti. Kenya ina jamii arobaini na nne tukiongezea jamii ya Wamakonde iliyotambuliwa 2017 na serikali ya Jamuhuri ya Kenya. Utachunguza mashairi ya awali na tenzi zilizozungumzia umoja wa jamii na mashairi ya hivi punde kutathmini iwapo utanzu huu unaweza kuendeleza au kuchangia umoja wa kitaifa nchini Kenya.

Maneno Muhimu: Ushairi, Utenzi, Shairi, Uzalendo, Utaifa, Umoja.

Utangulizi

Makala haya yatachunguza na kudadisi jinsi ushairi unavyoweza kutumika katika kuleta umoja wa kitaifa au utaifa na uzalendo nchini Kenya na nchi yoyote ile duniani. Ushairi una vipera vingi ikijumuisha mashairi, tenzi/tendi, ngonjera, malumbano na maghani. Kati ya vipera hivi, tutazingatia mashairi na tenzi zilizo katika maandishi. Tutateua baadhi ya tenzi na mashairi ambayo yanahimiza umoja katika nchi na yale ambayo, kama mtafiti, nayaona yanaweza kutumika kuhimiza umoja miongoni kwa watu wa jamii mbalimbali. Kwa hiyo uteuzi wake

ni wa kimakusudi. Tutachunguza ushairi huu kwa mtazamo wa kiuamilifu na KiMarx. Uamilifu (Emile Durkheim, Talcott, Radcliffe) unahimiza utamaduni au mchakato wowote katika jamii uchangie, kudhibiti na kuendeleza jamii (Odetola na Ademola, 1987; *Encyclopaedia Britannica* Vol.5). Mtazamo wa Kimarx unashadidia kauli kwamba fasihi yoyote inafaa kuyamulika masuala katika jamii na kutoa utatuzi au kuhamasisha jamii ambayo itatarajiwa kuyaona matatizo hayo na kuyatafutia utatuzi au suluhisho (Craig, 1975, Lodge, 1988). Kwanza nitafafanua dhana za ushairi, shairi na utenzi. Kisha tuchunguze jinsi vipera hivi vinaweza kutumika kuleta umoja na kujenga uzalendo hapa Kenya na kokote kule barani Afrika.

Dhana ya Ushairi

Kuna kauli anuwai za washairi walioelezea maana ya “ushairi”. Shaaban Robert katika utangulizi wa *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1962) alisema kwamba ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache. Hii ni kwamba ushairi ni sanaa ya vina na ufasaha wa maneno machache au maelezo yaliyotolewa kwa muhtasari na kuwekwa katika muundo wa nyimbo, mashairi wa tenzi. Mnyampala (1969) anaeleza kuwa ushairi ni kitu kilicho bora sana katika maongozo ya dunia na hutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangiliwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa shairi. Mambo mawili muhimu hapa yanaibuka. Kwanza ni kuwa ushairi una maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata. Pili, urari wa mizani na vina. Mulokozi na Kahigi (1975) wameeleza kuwa ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara, katika usemi, maandishi, au mahadhi ya nyimbo, ili kueleza wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani, kuhusu maisha au mazingira ya kibinadamu kwa njia inayogusa moyo. Kutokana na maelezo haya panaibuka mambo matatu muhimu;

- i) mpangilio maalum wa maneno fasaha na yenye muwala
- ii) lugha ya mkato inayoleta taswira mbalimbali zinzoleta mguso
- iii) mafunzo mbalimbali katika maisha ya binadamu

Massamba (1983) anaeleza shairi kuwa ni aina ya utungo ambao umekusudiwa kueleza hisi za ndani alizonazo msemaji au mshairi kwa kutumia lugha ya mkato au fupi, lugha yenye mvuto kwa namna maneno yake yaliyopangwa na kusarifiwa kwa uangalifu na ulinganifu, lugha yenye mguso wa moyo kwa ajili ya uzito wa maneno yake, lugha yenye mashiko na iliyo teuzi. Kwa muhtasari, ushairi ni aina ya utungo unaotumia lugha teuzi ya mkato na nzito yenye mnato iliyopangwa kwa uangalifu na ulinganifu kwa kueleza mawazo, tukio au hisi fulani ya mtunzi kuleta mafunzo na hata kutumbuiza huku yakiteka hisi za wasomaji au wasikilizaji. Katika ushairi, mtunzi lazima atumie maneno

mateule yanayoleta ridhimu na mdundo ambao unavutia na kuleta mguso kwa kuelezea maudhui yake. Huu ndio upekee wa utanzu huu tofauti na tanzu nyingine kama riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Hata hivyo, kuna tamthilia ambazo hutumia lugha ya kishairi.

Maana ya Utenzi na Shairi

Neno “utenzi” lina utata. Utenzi unaweza kufafanuliwa kwa mujibu wa umbo au maudhui. Baadhi wanahusisha utenzi na ushujaa, wengine na jambo zito au la kihistoria, wengine wanahusisha na mambo yasiyo ya kibinadamu, wengine umbo linalohusisha vina na urefu. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inaeleza utenzi kama utungo mrefu wa kishairi unaoelezea historia au kisa fulani ambao hauna vina vya kati katika mistari yake, bali kila ubeti una vyake isipokuwa mistari wa mwisho wa ubeti, yaani bahari. Hata hivyo kuna wataalamu wanaopambanua “utenzi” na “utendi”. Allen anaeleza kuwa “utendi” ni lahaja ya kaskazini yaani sehemu za Lamu, lakini maana ni ile ile ya mashairi ya matendo. Mulokozi (1989) anaeleza kuwa utendi ni shairi la matendo unaosimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Gibbe (1993) anaeleza umbo la utenzi hutumika kuelezea visa au matukio marefu au kutongoa jambo zito linalohitaji nafasi pana ya kulifafanua. Tukitazama umbo la utenzi tunapata kuwa lina mishororo mifupi yenye mizani kati ya 6 na 12. Mishororo hii haikugawika mara mbili, yaani haina ukwapi na utao. Utenzi una vina vya mwisho tu. Mfano:

Ambatana na adabu,
Uwe nayo karibu,
Ina mazao ajabu,
Shika usiache.

(Utenzi wa Adili, Shaaban Robert)

Hivyo, utenzi ni utungo mrefu ulioandikwa kishairi kuelezea visa au matukio marefu au jambo zito. Utenzi una mizani chache kuliko 12, na aghalabu hauna vina vya kati katika mishororo yake. Kila ubeti una vina tofauti japo hali hubadilika katika mishororo wa mwisho yaani bahari. Kwa hiyo, utenzi ni utungo unaosimulia ushujaa au matendo mengi ya kidini au ya kihistoria. Kuna mifano mingi ya tenzi za Kiswahili: Utendi wa Mwana Kupona (beti 97), Utenzi wa Hati (beti 100), *Utenzi wa Adam na Hawa* (beti 637), *Utenzi Rasi'IGhuli* (beti 4,583) n.k. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inaeleza shairi kama utungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo unaoeleza wazo au mawazo, hisi au tukio juu ya maisha na ambao hufuata utaratibu wa urari na muwala maalumu unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utenzi wa mashairi unaohusika. Tukizingatia wanamapokeo, shairi hutungwa katika umbo la beti, lugha teule ya mkato na mnato ili kuteka hisi, liwe na urari wa vina na mizani na mishororo iliyogawanyika mara mbili (ukwapi na utao) au

tatu (ukwapi, utao na mwandamizi). Pia liwe na muwala. Angalia mfano wa shairi lifuatalo:

Ulimwengu umbo lake, siku tatu ni tukufu
Ni mtu kuzawa kwake, ya pili ni maarufu
Ni mtu kuoja mke, ya tatu siku ya ufu
Na zote ni badilifu, kwa namna mbalimbali

(Malenga wa Mvita)

mwanzo ni tenzi au tendi zilizoandikwa. Mifano:

- i) Utendi wa Gilgamesh wa Kisumeria huko Mesopotamia.
- ii) Utendi wa Mahabharat huko India.
- iii) Tendi za Iliad na Odyssey za Homer huko Uyunani.
- iv) Wimbo wa Roland ambao ni utendi wa Ulaya.

Ushairi wa Kiswahili

Wataalamu mbalimbali, kwa mfano Amri Abeid, Shihabuddin Chiraghdin, Shaaban Robert, Massamba, Mulokozi n.k. waliofanya utafiti wa ushairi wa Kiswahili wanakubaliana kuwa chanzo cha ushairi wa Kiswahili ni nyimbo. Nyimbo hizo zilikuwa zikiimbwa katika ngoma za pungwa, vugo, harusi, chando, katika sherehe za jando na unyago, wakati wa kufanya kazi, hasa kazi zilipokuwa zikifanywa kwa ushirikiano au ujima, wakati wa kuwabembeleza watoto n.k.

Mwanzoni kabisa, nyimbo hizi zilikuwa hazifuati utaratibu maalumu lakini baadaye kukaja utaratibu wa kutumia vina na mizani kama ushairi ulivyo sasa. Kilichoanza ni utaratibu wa vina vya mwisho na baadaye vina vya kati. Washairi walipoanza kuandika ushairi, walitumia hati za Kiarabu. Historia inaeleza kuwa ushairi ulianza kuandikwa zamani sana kwa hati za Kiarabu huko Lamu. Wazungu walipowasili hapa Afrika ya Mashariki katika karne ya 19, ndipo mashairi yaliandikwa kwa hati hizi za Kizungu tuzijuazo. Washairi wa mwanzo walikuwa huko Lamu na Pate, kwa mfano, Fumo Liyongo (inadhaniwa aliishi kabla karne ya 12), Mwana Lemba (aliyeishi karne ya 17), Mwanakupona binti Mshamu (1790-1860), Seyyid Abdalla bin Nassir (1718-1815), Bakari bin Mwengo (1760-1830), Zahid bin Mngumi (1758-1828) na huko Mombasa kulikuwa na Ali Koti (1776-1834), Muyaka bin Haji (1776-1840), Mwalimu Sikujuwa bin Abdalla Batawi (1810-1889) n.k. (Rejelea: Chiraghdin na Nabahany, 1978). Katika karne ya 20, washairi mashuhuri wajulikanao ni Sheikh Amri Abeid, Shaaban Robert (1909-1962), Mathias Mnyampala, Ahmed Nassir (Malenga wa Mvita), Boukheit Amana (Malenga wa Vumba), Mwinyihatibu Mohamed (Malenga wa Mrima), Mwalimu Hassan Mbega, Musa Mzenga, Abdillatif Abdalla, Mulokozi, Kahigi, Massamba n.k. Hivi leo, ushairi wa Kiswahili umepiga hatua kubwa ambapo kuna mashairi ya kimapokeo na

kimapinduzi yanayoendelea kuandikwa kwa kuhifadhiwa. Washairi nao wamekuwa wengi na utanzu huu ungali unaendelea kukua.

Dhima ya Ushairi wa Kiswahili

Ushairi wa Kiswahili una dhima au kazi mahususi na nyingi. Wahakiki wa mwanzoni waliuangalia ushairi wa Kiswahili kama wenye dhima moja inayohusu maudhui ya dini ya Kiislamu. Hii ni kwa sababu ushairi wa mwanzo kuhifadhiwa ulikuwa tenzi/tendi zilizoandikwa na waislamu. Ukweli ni kwamba, ushairi wa Kiswahili umeweza kuhifadhi maudhui mengi na kuwa na dhima pana. Hata ukizichunguza tenzi hizo za kale, utagundua kuwa zina maudhui mbalimbali. Kwa ufupi, ushairi wa Kiswahili una dhima nyingi (Gibbe, 1978):

a) Kuwakemea dhulumati

Ushairi wa kale na hata wa leo huwakemea viongozi au watu wenye vyeo katika jamii wakiwadhulumu wenzao. Huwaonya watu kama hao waepukane na tabia ya kidhuluma. Mfano mzuri ni *Utenzi wa Al-Inkishafi* ulioandikwa katika karne ya 18. Utendi huu unawakemea viongozi wa Pate waliokuwa wakiwadhulumu wanyonge. Shairi la Abdulatif Abdalla “Mnazi Vuta N’kuvute” katika diwani yake ya *Sauti ya Dhiki* linakemea kiongozi anayewadhulumu wenzake baada ya kupigania uhuru pamoja. Yeye hupania kujinufaisha peke yake. Hali hii huwachosha na kuwaghadhabisha wenzake ambao daima hukumbuka azma ya kupigania uhuru. Hivyo, humtaka kiongozi huyo dhalimu kung’atuka mamlakani.

b) Kuakisi na kuhifadhi historia

Ushairi unaweza kutumika kuonyesha na kuhifadhi kumbukumbu za jambo lililotokea katika historia ya watu. Kwa mfano, *Utenzi wa Uhuru wa Kenya* uliotungwa na Salim Kibao unaeleza jinsi Kenya ilivyopigania uhuru wake, kando na kutoa orodha ya na wale waliohusika. Utendi huu unawasifu viongozi hao kwa kurejelea jitihada zao. Kwa njia hii, waliweza kuakisi historia ya miaka hiyo ya 50 ya vita vya uhuru na wakati huo huo kuhifadhi historia ya nchi ya Kenya katika ukombozi wake.

c) Kuliwaza

Ushairi wa Kiswahili ulitumika kuliwaza hasa wakati wa dhiki au msiba. Katika matanga ya Waswahili, mashairi yalisomwa ili kuwaliwaza na kuwapa moyo waliofiwa. Kwa mfano, *Utenzi wa Ras’lGhuli* wa Mgeni bin Faqhi ulikuwa ukisomwa katika matanga. Mashairi ya Ahmed Nassir (Malenga wa Mvita) “Kullu Nafsin Dhaaiqatul Mawt, Masikini Roho Yangu” ni mifano mizuri maliwazo.

d) Kutoa burudani

Asili ya ushairi ilikuwa ni kuburudisha. Binadamu wa mwanzo waliyatumia mashairi kutoa burudani baada ya kazi nyingi ya mchana kutwa. Wakati wa

mapumziko, waliyaimba mashairi kwa lengo la kujipa burudani na hivyo, kusahau uchovu waliokuwa nao. Hivi leo, mashairi huimbwa kumbini, shuleni na hata redioni ili kutoa burudani kwa hadhira au wasikilizaji.

e) Kuelimisha na kuzindua

Ushairi hutumika ili kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali. Siku hizi, kuna maradhi ya ukimwi yasiyo tiba na mashairi mengi yametungwa kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa huu. Shairi la Wamitila “Mwanamke” linaielimisha jamii dhidi ya kumdunisha mwanamke. Shairi la Abdala Kizere “Kila mwenye kuiza Kisomo” linaielimisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa sababu, yule anayepuza kisomo basi anajijengea ujinga na atakuja kujuta baadaye maishani mwake.

f) Kurunzi ya maisha ya mwanadamu

Ushairi huweza kuyamulika maisha ya mwanadamu jinsi anavyoishi. Mwanadamu huyo hutarajiwa kuaswa na kuadilishwa ili aache tabia fulani iliyo isiyopendeza. Kwa mfano, “Utendi wa Mwanakupona” unamwelekeza Mwanakupona kuhusu maisha kwa ujumla, na jinsi ya kuishi vyema ulimwenguni. Tenzi za Hati na Adili za Shaaban Robert ni mfano mzuri wa kazi ya kifasihi inayomwelekeza mwanadamu juu ya maisha ya mwanadamu hapa duniani na namna ya kuishi vyema.

g) Kuhimiza uzingatiifu wa dini

Tenzi nyingi za Kiswahili za mwanzoni zilisheheni maudhui ya kidini. Tenzi hizi zilimuamrisha mwanadamu kuyaandama yaliyo mema. Katika kufanya hivyo, pasina shaka, angeenda peponi atakapoaga dunia. Mara nyingi, tenzi hizi zilionesha uovu (Shetani) ukishindwa na wema (Mungu). Hapa, tuna mifano: Utenzi wa Ras’IGHuli, Utendi wa Tambuka. Mathias Mnyampala aliandika Utenzi wa Injili unaohimiza uzingatifu wa dini. Katika dhima hizi zote, makala haya yatajikita katika dhima za kuelimisha na kuzindua jamii ambapo ushairi unajitokeza kama kurunzi ya kuyamulika maisha ya mwanadamu.

Mchango wa Ushairi katika kuleta Umoja wa Kitaifa

Katika kuchunguza mchango wa ushairi, tutaanza na tenzi zinazochangia umoja wa wananchi. Kisha tutaangazia baadhi ya mashairi. Tezzi na mashairi haya yamejikita katika dhima ya kuelimisha na kuzindua jamii. Tenzi na mashairi ya watunzi wa Kenya na Tanzania yatumika kudhihirisha kwamba ushairi unaweza kutumiwa katika kuhimiza umoja hapa Kenya na kwingineko ulimwenguni.

Tenzi

Utenzi wa Uhuru wa Kenya (Salim Kibao, 1972) unatusimulia juhudi zilizofanywa na Wabunge wa Kiafrika nchini Kenya katika enzi ya ukoloni. Tenzi

hizi zililenga katika kumtetea mzee Jomo Kenyatta ambaye alikuwa amefungwa gerezeni. Tenzi hizi pia zilitetea uwezekano wa kukuza chama kimoja cha nchi nzima chenye kuwaunganisha wakenya. Kikubaliwe. Utenzi huu unahimiza umoja wa nchi. Tuchunguze baadhi ya beti hizi zinavyotusihi.

9. Ulivuka upinzani
 Ukaja serikalini
 Wakajiunga chamani
 Mambo yakaendelea
10. Kikawa chama kimoja
 Kiongozi ni moja
 Wala pasiwe na hoja
 Nchi tukatulia
28. Jambo kubwa kuungana
 Bila ya kubaguana
 Kwa wazee na vijana
 Tujiweke sawa sawa

Katika beti hizi tunaona vile nchi ilijitahidi kuwa na umoja utakaowawezesha kumuondoa mkoloni. Ingawaje kulikuwa na vyama mbalimbali (KANU na KADU, n. k), juhudi ziliwekewa muungano wa Wakenya. Chama kimoja kikakuzwa na baaadaye, kukatokea /kiongozi mmoja. Watu wote waliridhia bila manung'uniko.

50. Tukakutana wa Pwani
 Kwa pamoja uwanjani
 Kusikiza kwa makini
 Hayo waliyoitiwa.
51. Mzee akatamka
 Umoja tunautaka
 Kamba moja kuishika
 Kwa pamoja sote pia.

Beti hizi vile vile tunaona Mzee Jomo Kenyatta akihimiza umoja.

648. Mzee akawapokea
 Naye akawaambia
 'Sote tumefurahia
 Ndugu zetu kutujia'.
649. 'Tumefurahia sana
 Kwa vile mlivyoona
 Ubora ni kupatana
 Kwa Wabunge wote pia'.

835. Lazima tuwe tayari
Na kuweza kusubiri
Subira huvuta heri
Kama tunavyoona.
836. Kamba moja tuishike
Ya harambee tusichoke
Waume na wanawake
Pasiwe wa kulegea.
837. Tukishikana pamoja
Tukawa ni nguvu moja
Kila kitu kitakuja
Mudawe ukiwadia.

Beti hizi zinaonyesha viongozi wetu walivyohimiza umoja kwa nia ya kuendeleza umoja na maendeleo ya nchi. Umoja unaonwa kama nguzo muhimu sana kwa maendeleo ya. Nchi iliyogawanyika hukosa maendeleo. Matokeo yake ni vita na nchi kurudi nyuma. Umoja ni kitu adhimu.

“Utenzi wa Kenya”

Utenzi wa Kenya uliandikwa na Karama (1985) katika Diwani yake *Urembo wa Kiswahili*. Utenzi huu unazungumzia masuala ya kimsingi kuhusu taifa la Kenya. Mojawapo ya masuala haya ni umoja wa wananchi wa taifa la Kenya. Karama anahimiza umoja, kama ubeti ufuatao unavyodhihirisha:

Ubeti 24: Na sasa ndivyo yataka
Hima tufanye haraka
Sote tuwe ni shirika
Umoja ndio sheria. (msisitizo ni wangu)

Kutokana na pendekezo hili la Karama, sheria inafaa kupenyezwa kwenye Katiba yetu, hivi kwamba yeyote anayembagua Mkenya mwenziwe kwa misingi ya aina yoyote ile, atafaa kufikishwa mahakamani. Sheria hii itasaidia sana.

Mashairi

Kuna mashairi yanayohimiza umoja. Mashairi haya yaliandikwa na Wakenya katika miaka ya nyuma. Mmoja wao ni Boukheit Amana (1982). Shairi lake "Vijana linden Nchi" linahimiza umoja:

Tuunganeni vijana, ili tugawane kazi
Wazee nguvu hawana, mazito hatuyawezi
Bora kubadilishana, nanyi vichanga vizazi.

...

Toka pwani hadi bara, vijana nchi linden,
Tokeni muwe imara, hasa humo mipakani,

Ajaribuye kupora, vijana mchafueni.
Onyesheni uzalendo, washituke vibaraka,
Muonyeshe kwa vitendo, na nia zilizosafika,
Mujivune na mwenendo, tamaa ya madaraka.

(uk. 85-86)

Beti hizi zinasisitiza umoja wa vijana ambao wanashauriwa kuwa imara katika kuilinda nchi. Vijana wote nchini wanapewa ujumbe huu. Ujumbe unatolewa kwa ufasaha kwa kutumika lugha nzito, inayovutia na iliyo wazi. Vijana wanahimizwa wasiwakubali viongozi fisadi kama beti zifuatazo zinavyoshauri: "Ajaribuye kupora, vijana mchafueni". Huu ni ujumbe mzito sana kwa vijana nchini. Iwapo Wakenya watazingatia wosia huu, pasina shaka, umoja utapatikana. Umoja huu una masharti kama anenavyo Amana katika shairi hili: "Heshima ya Serikali":

Mkusanyiko wa umma, ni mpango wa Jalali,
Jalali mwenye huruma, aloumbwa kila mwili,
Mwili wa mtu na nyama, akatia na akili,
Akili yenye kupima, la hali na batili,
Batili haina wema, iwapo hapo kalili.

Kalili huwa imara, iwapo na kiongozi,
Kiongozi wa busara, asiye na ubaguzi,
Ubaguzi ni hasara, isofaa siku hizi,
Siku hizi za fikara, za watu wanaomaizi,
Kumaizi hali bora, yasiyo na pingamizi.

Pingamizi kuzing'owa, baina yetu raia,
Raia tukateuwa, serikali ya jamia,
Jamia tukaridhiwa, kuwa haina udhia,
Udhia tukiletewa, tusiridhi vumilia,
Kuvumilia kwauwa, hasa kumwasi Jalia.

(uk. 85)

Beti hizi zinaeleza umoja unaotokana na uwezekano wa kuwachagua viongozi. Kiongozi huyu anatakikana kufanya haki nchini kwa nia ya kudumisha umoja. Pasina haki, umoja utakuwa ndoto. Kwa hivyo, umoja huweza kukuzwa na kuimarishwa na viongozi bora wanaotawala nchi katika misingi ya maadili. Shairi lifuatalo linadumu kwa muda mrefu. Viongozi wa wakati wowote ule wanapewa wosia unaowahimiza kudumisha umoja nchini. Aidha katika shairi "Nyama huyu Kabaila" Amana (1983:82-83), mtunzi anaushutumu ukabila na kuhimiza umoja miongoni mwa Wakenya. Anadai kuwa tulikuwa na umoja lakini mnyama huyu "kabila" alipoingia miongoni mwetu, umoja ukabomoka. Kwa

hivyo, Amana kwa kukemea ukabila anahimiza umoja nchini. Tuchunguze beti hizi:

Howe! Napiga unyende, musikie wakulima
Wakulima kila pande, nipulikani kwa hima
Humu mwenye letu bonde, mumeingia mnyama
Metuvamia mnyama, nyama huyu kabaila.

Ndugu njooni karibu, tulinganishe kalima
Tufanyeni taratibu, za kumtowa mapema
Asije akaharibu, mazao yetu ya wema
Ni muharabu wa wema, nyama huyu kabaila.

...

Kabaila nyama mui, mnyama aso huruma
Muovu aula chini, si mwema katu si mwema
Huyu kwetu ni adui, shamba letu tulichoma
Kiunga atakichoma, nyama huyu kabaila.

Tukitaka tuokoke, njia moja ya hekima
Ni kuwa tujumuike, kwa umoja wakulima
Kisha tumshake-shake, mnyama apate tama,
Tumshakapo tatami, nyama huyu kabaila.

Kumfurusha ndo dawa, tutakapo usalama,

...

Amana ametumia jazanda kadhaa katika shairi hili. Ametumia jazanda ya “bonde” kusimamia “nchi” na ya “wakulima” kusimamia “wananchi”. Anatutahadharisha kwamba nchi imeingia mnyama mbaya aitwaye “Ukabila”. Ukabila huu anasema ni uharibifu na unaondoa wema nchini. Na hatimaye, utaleta utengano (shamba letu talichoma). Kwa hivyo ni adui mkubwa kwetu na ni lazima tuungane kwa sauti moja kuukemea ukabila. Ili hili litimie, Amana anatueleza: Tukitaka tuokoke, njia moja ya hekima,

Ni kuwa, tujumuike, kwa umoja wakulima,

...

Abdilatif Abdalla (1973:36-41) katika shairi lake “Mamaetu Afrika” anazungumzia jinsi Wakoloni walivyofilisi Bara la Afrika. Katika mjadala huu vile vile anahimiza umoja na uzalendo. Tuchunguze beti hizi:

19. Japo twali mbalimbali, kila ukoo pekee
Tukaona afadhali, kila tapo lisongee
Kila pembe na mahali, adui tumlemee
Wana na walo wazee, tukawa vitani Mama.

34. Badala ya kuungana, tuwe ni kitu kimoja
Tupate shirikiyana, sisi na wao pamoja
Tukulinde san asana, kwa kila litakalokuja
Bali wao yao haja si sawa na yetu Mama.
38. Tu tayari damu yetu, kwa mikondo imwaike
Tu tayari roho zetu, kwa maelfu zitoke
Tukuhami Mamaetu, kila baya likwepuke
Hishimayo tuiweke, Afrika wetu Mama.

Katika beti hizi, Abdilatif anatufahamisha umuhimu wa umoja wa makabila mbalimbali na ule wa vijana na wazee. Hapo zamani, enzi za kupigania uhuru, Waafrika (Wakenya wakiwemo) waliungana na kuwa kitu kimoja. Kwa nini basi, sasa hivi tutengane? Nia ikiwepo na viongozi wasisitize umoja nchini kwa vitendo vya dhati na kwa kuamini, umoja na uzalendo hapa Kenya tutaaurudisha. Tutakapo kuwa na uzalendo huu, utaifa utazaliwa na tutarudisha heshima kwa nchi yetu machoni mwa ulimwengu. Mulokozi na Kahigi (1975) katika shairi “Wimbo wa Moyo” katika kitabu chao Kunga za Ushairi na Diwani Yetu wanatueleza haya:

Njoo hapa tuketi pamoja
katika uwanja wa ujana na mpevu
Njoo hapa tuimbe pamoja
katika uwanja wa majani mabichi
Chini ya mwembe huu
wenye matunda mabivu.

Katika ubeti huu, kunahimizwa umoja kati ya vijana na wazee. Watu wawe pamoja katika nchi zetu changa (sasa ni komavu) na zenye utajiri. Watunzi hawa wametumia jazanda ya “uwanja” na “mwembe” kusimamia “nchi” na “matunda mabivu” ni “rasilimali au utajiri” wa nchi. Tutakapokuwa na umoja sote tutafurahia utajiri wetu.

Hitimisho

Kutokana na mifano niliyotoa, ni dhahiri ushairi unaweza kutumika kuleta umoja nchini. Ujumbe wake ni mzito. Lugha ni sahili na yakuvutia. Kila asomaye tungo hizi anafahamu yanayozungumziwa na kuhimizwa, kutoka kwa wananchi hadi kwa viongozi. Litakikanalo ni juhudi ya kufikisha ujumbe huu kwa wote. Mashairi yanavutia sana sana hususan yanapoimbwa. Kwa hivyo mashairi yanayohimiza uzalendo na umoja yaimbwe redioni na katika runinga wananchi waburudike na kupata ujumbe unaotolewa. Aidha katika sherehe za kitaifa hapa nchini mashairi na nyimbo zipewe kipaumbele katika kutoa burudani kwa hadhira. Ujumbe upatikanao ufuatilizwe na vitendo hasa na viongozi wetu.

Jambo lolote kufanyika tunahitaji mfuatuzi, yaani jambo lizungumzwe kila mara. Mashairi yatumike kwa kuimbwa, kusomwa na kuandikwa yakihimiza umoja. Ushairi uingizwe katika mtalaa wa shule za msingi na sekondari uwe lazima katika vipindi vya somo la Kiswahili na Kiingereza. Mashairi yawe yale ya kuhimiza umoja nchini. Nina hakika, tukianza mchakato huu kutoka darasa la kwanza hadi kidato cha nne, wanafunzi wanahimizwa umoja kupitia ushairi, azma yetu ya umoja, uzalendo na utaiifa itatimia na kufaulu. Sote tutajivunia kuwa Wakenya na ndugu.

Marejeleo

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: O.U.P
- Amana, B. (1982). *Malenga wa Vumba*. Nairobi: O.U.P
- Abeid, A. K. (1962). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*, Dar es Salaam: The Eagle Press.
- Allen, J. W. T. (1971). *Tendi*. Nairobi: Heinemann
- Chacha, N. C. (1987). *Meaning and Interpretation of Swahili Poetry: A Portrayal of a Changing Society*. PhD Thesis, Yale University *Encyclopaedia Britannica* Vol.5
- Finnegan, R. (1975). *Oral Poetry*. London: O.U.P
- Gibbe, A. (1978). "Dhima ya Fasihi katika Jamii" ktk *KISWAHILI Vol.47*. Dar es Salaam:TUKI. uk. 24-38
- Fischer, E. (1953). *The Necessity of Art*, London, Penguin Books Ltd
- Gilbert, A. H. (1962). *Literary Criticism: Plato to Dryden*, Detroit: Wayne State University Press.
- Karama, S. (1985). *Urembo wa Kiswahili*, Nairobi: Evans Brothers Ltd.
- Kibao, S. A. (1983). "Namna ya Kujifunza, Kuliandika na Kulifumbua Shairi la Kiswahili" *FASIHI*, 96-113, Dar es Salaam: TUKI.
- Kibao, S. A. (1974). *Utenzi wa Uhuru wa Kenya*. Nairobi: O.U.P
- Mulokozi, M. M na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Dar es Salaam: T.P.H.
- Olatunde T. na Ade, A. (1987). *Sociology: An Introductory African Text*, London: Macmillan.